JIMBO KUU KATOLIKI DAR ES SALAAM



MPANGO MKAKATI WA HALMASHAURI YA WALEI 2023 – 2026

Imeandaliwa na:

Halmashauri ya Walei

Jimbo Kuu la Dar es Salaam

Septemba, 2023

VIFUPISHO

JNNK	=	Jumuiya Ndogo ndogo za Kikristu
VMJ	=	Vyama, Mashirika na Jumuiya za Kitume

Maana ya Misamiati

Walei: Ni waamini wote, ukiondoa Makleri na wale wenye maisha ya wakfu

Makleri: Wapakwa mafuta katika Kanisa Katoliki

Watawa: Ni watu waliojitenga kimaisha ya kawaida ili kuishi maisha maadilifu

Hierakia: Ngazi za Mamlaka ya kiutawala katika Kanisa Katoliki

WAWATA: Ni chama cha kitume cha Wanawake Wakatoliki Tanzania

UWAKA: Ni chama cha kitume cha Umoja wa wanaume Katoliki Tanzania

VIWAWA: Ni chama cha kitume cha Vijana Wafanyakazi Wakatoliki Tanzania

Halmashauri ya Walei: Ni chombo cha kitume kinachounganisha Waamini Walei katika wito na utume wao wa kutakatifuza malimwengu katika ngazi zote kuanzia JNNK hadi Taifa

YALIYOMO

VIFUPISHO 2
YALIYOMO 4
SURA YA KWANZA 5
1.0 UTANGULIZI 5
1.1 MKABALA (Approach) 5
1.2 MPANGILIO (Layout of the Plan) 5
SURA YA PILI 7
2.0 UCHAMBUZI WA HALI ILIVYO HADI SASA (Situational Analysis) 7
2.1 Chimbuko la Baraza na Halmashauri ya Walei 7
2.2 Kuanzishwa kwa Baraza la Walei 7
2.3 Kuanzishwa kwa Halmashauri ya Walei 7
2.4 Halmashauri ya Walei Mwaka 2023 7
2.5 Mapitio ya Mpango Mkakati ulioisha 7
2.5.1 Mafanikio kwa Kipindi kilichopita cha 2020 - 2023 8
2.5.2 Masuala yaliyoibuka/Changamoto kwa kipindi cha 2020 - 2023 8
2.5.3 Fursa zilizokuwepo na zinazoendelea kuwepo 9
2.5.4 Masuala ya Msingi yenye kupewa kipaumbele 9
SURA YA TATU 10
3.0 MPANGO MKAKATI 10
3.1 DIRA, DHIMA, KAULIMBIU NA MAADILI 10
3.1.1 Dira 10
3.1.2 Dhima 10
3.1.3 Kaulimbiu 10
3.1.4 Maadili 10
3.2 MALENGO YA MPANGO MKAKATI 2020 HADI 2023 11
3.2.1 Dhana ya Mpango Mkakati (Rationale) 11
3.2.2 Mpango Mkakati na Malengo Mahsusi ya utekelezaji 12
SURA YA NNE 26
4.0 MPANGO WA FEDHA NA MAKISIO 26
4.1 Makisio ya mapato na matumizi 26
4.2 Ufuatiliaji na Tathimini 26

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Jimbo Kuu la Dar es Salaam (kwa Kilatini Archidioecesis Daressalaamensis) ni mojawapo kati ya majimbo 34 ya Kanisa Katoliki nchini Tanzania. Chini yake kuna kanda ya Kanisa yenye majimbo matano ambayo ni: Zanzibar, Tanga, Morogoro, Mahenge na Ifakara. Jimbo hili lilianzishwa kama Apostolic Prefecture kutoka Apostolic Vicariate ya Nairobi mnamo tarehe 16 Novemba, 1887. Mnamo tarehe 15 Septemba, 1902 lilipandishwa hadhi na kuwa Apostolic Vicariate ya Dar es Salaam, na tarehe 25 Mach 1953 lilifanywa kuwa Jimbo Kuu. Kwa sasa, Jimbo linaongozwa na Askofu Mkuu Yuda Thaddeus Ruwa'ichi tangu 2019.

Mpango Mkakati ni mwongozo unaoonesha njia ya kufikia dira au ndoto inayokusudiwa na taasisi husika na namna gani itafikia kwa kipindi fulani kijacho. Mpango Mkakati unaonyesha malengo makuu, malengo ya kiutendaji, viashiria vya matokeo na mhusika katika kusimamia utekelezaji.

1.1 MKABALA (Approach)

Uandaaji wa Mpango Mkakati huu ulihusisha Wajumbe wote wa Halmashauri ya Walei ya Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam. Wajumbe hawa wanatoka katika Parokia 159 zinazounda Jimbo; Mashirika ya Kitume na Vyama vya Kitume ngazi ya Jimbo kwa lengo la kuwa na mpango ulioshirikishi.

1.2 MPANGILIO (Layout of the Plan)

Mpangilio wa uandaaji Mpango Mkakati huu unahusisha Sura nne na Viambatisho.

Sura ya Kwanza ni Utangulizi unaoelezea mkabala (Approach) na mpangilio.

Sura ya Pili inaongelea mchanganuo wa hali ambayo kanisa limepitia na sehemu lilipofika, Mafanikio na Changamoto tulizopitia. Aidha, Majukumu na kazi za Halmashauri zilizopo zinaelezwa katika Sura hii pamoja na mambo muhimu yanayohitaji kufanyiwa kazi.

Sura ya tatu ni Mpango wenyewe. Unaelezea Dira, dhima, maadili ya msingi na malengo ya Halmashauri. Malengo ya utendaji yanaainishwa katika Sura hii pamoja na viashiria vya utendaji.

Sura ya nne inaelezea mfumo wa bajeti na Ufuatiliaji na Tathmini. Na mwisho ni Majedwali. Jedwali la kwanza linahusu Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini. Jedwali hili linaonesha: viashiria vya utendaji; maelezo ya kiashiria; takwimu za msingi na namna ya ukusanyaji wa takwimu wakati wa ufuatiliaji. Jedwali la pili linahusu Utekelezaji wa

Mpango ambapo malengo, malengo ya kiutendaji, viashiria vya utendaji na mhusika vimeainishwa.

SURA YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA HALI ILIVYO HADI SASA (Situational Analysis)

Sura hii inajaribu kuchambua namna Halmashauri ilivyobuniwa na kuanzishwa awali. Sababu za kubuniwa kwake na majukumu yake.

2.1 Chimbuko la Baraza na Halmashauri ya Walei

Mtaguso Mkuu wa Pili wa Vatican uliofanyika kati ya tarehe 11 Oktoba 1962 hadi 8 Desemba 1965 ulitoa tamko kuhusu “Harakati za Kitume” (Apostolicam actuositatem) kwa kutambua mchango wa waamini walei katika maisha na utume wa Kanisa na hasa nyakati hizi za utandawazi na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Waliwataka waamini walei kutambua kwamba, wanashiriki kikamilifu huduma za Kristo za kikuhani, kinabii na kifalme. Waamini walei wanahamasishwa kushiriki kwa dhati kabisa, maadhimisho ya Sakramenti za Kanisa na hasa Sakramenti ya Ekaristi Takatifu, chanzo na kilele cha maisha na utume wa Kanisa.

2.2 Kuanzishwa kwa Baraza la Walei

Baada ya Mtaguso huu Baraza la Walei lilianzishwa mwaka 1969 na Hayati Askofu James Sangu aliyekuwa Mwenyekiti Idara ya Utume wa Walei, Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania.

2.3 Kuanzishwa kwa Halmashauri ya Walei

Mnamo mwaka 1983 Baraza lilifanyiwa marekebisho na kuitwa Halmashauri ya Walei Tanzania.

2.4 Halmashauri ya Walei Mwaka 2023

Halmashauri ya Walei Jimbo Kuu la Dar es Salaam kwa sasa inaundwa na Kamati Tendaji za Halmashauri za Walei za Parokia 159 pamoja na Wenyeviti wa Vyama, Mashirika na Jumuiya za Kitume (VMJ) ngazi ya Jimbo. Uongozi ndani ya Halmashauri ya Walei ni kwa mujibu wa Katiba ya Walei Katoliki Tanzania ambapo viongozi wake huchaguliwa na kudumu kwa kipindi cha miaka mitatu.

2.5 Mapitio ya Mpango Mkakati ulioisha

Katika Mpango Mkakati wa miaka mitatu iliyopita, (2020-2023), Halmashauri Walei Jimbo iliandaa Mpango Mkakati ambao ulitekelezwa kwa ufanisi mkubwa, mpango huo ulitekelezwa chini ya Uongozi wa Padre Vitalis Kassembo Mkurugenzi wa idara ya Walei Jimbo.

2.5.1 Mafanikio kwa Kipindi kilichopita cha 2020 - 2023

i) Ushirikiano na Wakreli na taasisi nyinginezo mbalimbali katika vipindi tofauti kadiri ya mahitaji yalivyokuwa yakiainishwa.
ii) Kila Parokia iliweza kuongeza idadi ya waamini katika masakramenti ya ubatizo, kipaimara, ndoa na nyinginezo.
iii) Mikutano katika ngazi mbalimbali ilifanyika kama ilivyokuwa imepangwa
iv) Parokia nyingi za Jimbo la Dar es Salaam zilianzisha na kuendesha miradi mbalimbali ya maendeleo na ya Ujenzi, ambapo makanisa na parokia mpya **34** zilifunguliwa.
v) Kuwa na vyanzo na mbinu mbalimbali za kuongeza mapato.
vi) Kushiriki mikutano, hija na makongamano mbalimbali ndani na nje ya Jimbo
vii) Kuweza kulipa michango yote ya ndani na ile ya nje Kijimbo, licha ya Changamoto ya tatizo la ugonjwa Corona, Hija za Ndani ya Jimbo na nchi za nje zimeendelea kufanyika.
viii) Ushiriki kwa kusaidia uinjilishaji katika Parokia za Pembezoni; Mafia, Kisiju, Utete, Kibiti, Ikwiriri na Kisarawe.
ix) Kuendesha makongamano makubwa ya Injili yaliyoendeshwa kupitia vyama, mashirika na jumuiya mbali za kitume jimboni
x) Kufanikisha uchangiaji kusaidia uendeshaji wa Seminari ya Visiga kupitia WAWATA
xi) Kusaidia uchangiaji wa kusaidia Wadada wadogo kupitia UWAKA
xii) Kusaidia kufaniniksha ujenzi wa Groto Pugu kupitia UWAKA na WAWATA
xiii) Kufanikiwa kuandaa Warsha mbalimbali za Waamini katika Jimbo kila Mwaka.

2.5.2 Masuala yaliyoibuka/Changamoto kwa kipindi cha 2020 - 2023

1) Kulala kwa Imani Katoliki na baadhi ya waamini kuwa na kiu ya kumtafuta Mungu kwa kupapatikia mahubiri ya wachungaji wanaojinasibu wanafanya miujiza, wana maji na mafuta yanayoweza kuwaponya na maradhi mbalimbali.
2) Jumuiya na Mitaa mingi inazungukwa na mchanganyiko wa imani za dini ya Kiislamu na Madhehebu mengine ya Kikristo ambayo kwa asili yake ni changamoto kwa Kanisa Katoliki;
3) Uwajibikaji hafifu kwa baadhi ya viongozi wa ngazi mbalimbali za Walei kuanzia Jumuiya, vigangoni hadi maparokiani kunakosababishwa na kutokuijua Katiba ya Halmashauri ya Walei Tanzania na kuitumia katika majukumu yao ya kila siku;
4) Udhaifu katika ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu katika baadhi ya parokia, hivyo kushindwa kuwa na Takwimu kamili za waamini katika maeneo yao;
5) Mahudhurio hafifu katika mikusanyiko kwa baadhi ya JNNK na hasa Wanaume, vijana na watoto
6) Maisha ya waamini wengi ni duni na uchumi mdogo.

7) Utata wa eneo la mipaka kwa baadhi ya Parokia za Jimbo la Dar es salaam
8) Baadhi ya Parokia kukosa miradi ya kiuchumi kwa ajili ya maendeleo ya Parokia na hivyo kutegemea michango toka walei kwa kila jambo
9) Kuibuka kwa magonjwa ya kuambukiza kama corona yaliyopunguza mahudhurio na utoaji michango mbalimbali
10) Wafanyakazi wengi katika maparokia kukosa mikataba ya kazi na hivyo kufanya kazi kwa manunguniko
11) Waumini wengi kuishi bila ndoa takatifu/Ndoa mseto
12) Kukosa kalenda ya matukio mbalimbali katika baadhi ya Parokia na hivyo kuathiri kumbukumbu ya kutekeleza baadhi ya mambo muhimu kwa wakati.

2.5.3 Fursa zilizokuwepo na zinazoendelea kuwepo

i) Uwepo na utayari wa Mapadre kuhudumia waamini katika parokia zote jimboni
ii) Uwepo wa vyama vya kitume vinavyosaidia kuleana kiroho na kukoleza Imani
iii) Uwepo wa Katiba ya Halmashauri ya Walei, Biblia ya Wakatoliki, Mtaguso Mkuu wa pili wa Vaticano na Katekisimu Katoliki
iv) Uwepo wa Mfumo wa ngazi za uongozi kuanzia JNNK hadi Jimboni
v) Utaratibu wa vikao katika ngazi za uongozi kuanzia JNNK hadi Jimboni

2.5.4 Masuala ya Msingi yenye kupewa kipaumbele

Ili kuendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizopo, Halmashauri ya Walei Jimbo, na kwa kuzingatia vipindi vya uongozi vya miaka mitatu mitatu katika madaraka tumeandaa Mpango Mkakati wa miaka mitatu kuanzia Julai 2023 hadi Juni 2026 kama njia ya kukabiliana na changamoto pia kurahisisha uongozi wa pamoja ulio na mahali pa kusimamia na kurejea.

i) Kuimarisha mafundisho ya Biblia kwa waamini
ii) Kuimarisha mafundisho ya dini mashuleni, kwenye Jumuiya na kuinua ari ya kuishi Katekisimu Katoliki
iii) Kuimarisha uwezo wa utendaji kwa vyama vya kitume, Mashirika na Jumuiya katika ngazi ya Jimbo na Parokia.
iv) Kuongeza uelewa kwa viongozi wa Parokia na Jimbo katika masuala mbalimbali ya Ujasiriamali na uchumi ili kuwasaidia Walei katika ngazi mbalimbali
v) Kuwezesha semina za ujasiliamali kwa waamini ili wapate elimu kukuza uchumi wao.
vi) Kuendesha na kuongeza vitega uchumi vya Halmashauri ya Walei
vii) Kuwezesha Parokia zilizo pembezoni na zimezunguukwa na watu wengi wa Dini tofauti na Katoliki

SURA YA TATU

3.0 MPANGO MKAKATI

Sura hii inaelezea Mpango utakavyotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2023 hadi 2026. Kauli za kiwango cha juu ambazo ni dira na dhima zimeainishwa pamoja na maadili ya msingi na malengo ya Mkakati huu.

Kwa mujibu wa Katiba ya Halimashauri ya Walei (2019), kumeainishwa Dira, Dhima na Kaulimbiu ili kuweka mwelekeo wa majukumu na uwajibikaji ndani ya shughuli za uendeshaji wa Halmashauri ya Walei.

3.1 DIRA, DHIMA, KAULIMBIU NA MAADILI

Kwa mujibu wa Katiba ya Halmashauri ya Walei (2019), kumeainishwa Dira, Dhima, Kaulimbiu na Maadili ili kuweka mwelekeo wa majukumu na uwajibikaji ndani ya shughuli za uendeshaji wa Halmashauri ya Walei.

3.1.1 Dira

Kuwa kitovu cha ubora cha kuishauri ipasavyo Hierakia katika ngazi husika za Halmashauri kuanzia Jumuiya ndogo ndogo, Parokia, Dekania, Jimbo hadi Taifa katika safari ya kulipeleka Kanisa Mbinguni.

3.1.2 Dhima

Kuwaunganisha Waamini Walei katika Wito na Utume wao wa kutakatifuza malimwengu kwa ajili ya Kristo katika ngazi husika kuanzia Jumuiya Ndogondogo hadi Taifa

3.1.3 Kaulimbiu

Nuru yetu iangaze ili tutakatifuze malimwengu

3.1.4 Maadili

Maadili ya Msingi Katika kutekeleza Dhima iliyotajwa hapo juu ili itufikishe kwenye Dira yetu, Halmashauri itatumia maadili ya msingi yafuatayo:

a) Kutenda kwa wajibu na haki;

b) Kushuhudia imani kwa ujasiri na ukweli;

c) Kudumu katika sala na neno la Mungu; na

d) Kuimarika kiroho.

3.2 MALENGO YA MPANGO MKAKATI 2023 HADI 2026

Yafuatayo ni malengo manne (4) yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati huu yatakayohitaji utekelezaji ili kufikia Dira ya Halmashauri na kujibu changamoto zilizoonekana kipindi kilichopita.

A: Kuimarisha IMANI ya waamini Walei.

B: Kuimarisha utendaji wa Halmashauri ya Walei katika ngazi zote za uongozi.

C: Kubuni mipango ya kimaendeleo na kuratibisha mambo yanayohusu mipango, uchumi na fedha.

D: Kuimarisha ufuatiliaji na tathimini ya malengo ya Mpango Mkakati.

3.2.1 Dhana ya Mpango Mkakati (Rationale)

Waamini wengi wana hamu ya kumjua Mungu na kuhitaji kuimarishwa kiroho kwa kuliishi neno la Mungu na Mapokeo ya Kanisa kama msingi wa kuwapeleka mbinguni na wanahitaji mahubiri ya aina mbalimbali pamoja na masomo yanayohusu Neno ili waweze kupata mwanga na kuimarika zaidi pamoja na kumjua Mungu zaidi.

Mafundisho ya Katekisimu Katoliki na mafundisho ya dini mashuleni pia yamekuwa ni changamoto kutokana na idadi kubwa ya shule na watoto kwa kulinganisha na walimu wa dini kwenda kufundisha. Uelewa wa majukumu yaliyoainishwa kwenye katiba ya Halmashauri ya walei nalo ni eneo linalohitaji mkazo zaidi pamoja na elimu ya ujasiliamali kwa waamini.

3.2.2 Mpango Mkakati na Malengo Mahsusi ya utekelezaji

Mpango Mkakati wa kwanza
Kuimarisha IMANI ya waamini Walei.

Mkakati (Strategies)

- Kuimarisha Maisha ya kitakatifu miongoni mwa walei kwa kuwahimiza kusoma neno la Mungu, Katekisimu ya Kanisa Katoliki, Mtaguso mkuu wa pili wa Vatikani na nyaraka mbalimbali za kanisa.
- Kuongeza uelewa kwa waamini Walei kuhusiana na malezi, familia na afya kufikia kiwango cha juu.
- Kuongeza uelewa kwa waamini Walei katika masuala yanayohusu Haki, Amani, Ulinzi, Usalama na Mazingira.
- Kuhimiza ufundishaji wa Elimu ya Dini Mashuleni na Vyuoni
- Kuratibisha mafundisho ya elimu ya Dini baada ya Kipaimara
- Kuimarisha uinjilishaji kwa parokia zilizo pembezoni kwa lengo la kukuza Imani Katoliki

Malengo Mahususi (Targets)

- Uwepo wa vikundi vitatu vya kujifunza kwa undani mafundisho ya kanisa katoliki kwa kila Parokia
- Idadi ya waamini wanaofuatilia Vyombo vya Habari vya kanisa kufikia kiwango cha juu
- Kuimarisha miundo mbinu ya maeneo ya huduma za Kiroho kama maeneo ya Hija, Makanisa na Vituo vya sala
- Kuendesha semina 2 kwa mwaka zenye lengo la kuboresha uelewa kuhusiana na masuala ya malezi, familia na afya
- Kuhamasisha waamini kufuatilia vyombo ya Habari vya kanisa.
- Kuhamasisha waamini Walei kuwa kuwa na tiba kinga na bima za afya.
- Kuimarisha makundi mbalimbali ya uinjilishaji kama vile vyama vya kitume, Vijana na kamati sizizo za kikatiba kwa njia ya semina 2, Hija 2 na Mafungo 2 kwa mwaka
- Utoshelevu wa mafundisho ya Dini mashuleni na vyuoni kufikia kiwango cha juu
- Kuwatambua walimu wakatoliki Wastaafu na wasiowastaafu walio waadilifu kwa kila Parokia na kuwajengea uwezo wa kufundisha Elimu ya Dini.
- Kutoa Mafundisho endelevu ya Dini kwa watoto wote waliopata Kipaimara.
- Kufanya ziara za uinjilishaji 4 kwa mwaka kwa kila Parokia za Pembezoni

Viashiria vya Utendaji (Key Performance Indicators)

- Kupungua kwa idadi ya waamini walei wanaoihasi Imani Katoliki
- Kuongezeka kwa idadi ya waamini wakatoliki
- Kuongezeka kwa Idadi ya Parokia
- Kuimarika Zaidi kwa Imani ya waamini Walei na kuongezeka kwa miito mitakatifu
- Kuongezeka kwa idadi ya washiriki kwenye Hija, Semina, warsha, mafungo na makongamano
- Kuongezeka kwa idadi ya waumini wanaoshiriki sakramenti mbalimbali za kanisa
- Kuongezeka kwa idadi ya waamini wanaofuatilia vyombo vya Habari vya kanisa.
- Kuendelea kwa kituo cha Hija Pugu na kuwekeza kwa shughuli za kiibaada.
- Kuongezeka kwa idadi ya Makanisa/Parokia.
- Kuimarika kwa maadili miongoni mwa waamini walei
- Kuongezeka kwa idadi ya wanandoa wanaotumia mpango wa uzazi wa asili.
- Kuongezeka kwa waamini wanaofuatilia Habari za kanisa kufikia kiwango cha juu
- Kuongezeka kwa idadi ya waamini walei wenye bima ya afya kufikia kiwango cha juu
- Kupungua kwa idadi ya waamini wanaoishi Maisha ya unyumba bila sakramenti ya ndoa kwa kiwango cha juu.
- Kupungua kwa magonjwa yasioambukizwa miongoni mwa waamini walei kwa kiasi kikubwa.
- Kuongezeka kwa idadi ya vikundi vya uinjilishaji
- Kuongezeka kwa uelewa wa waamini katika mambo ya Haki wajibu na sheria.
- Mafundisho ya dini mashuleni kufanyika kwa mujibu wa ratiba
- Kuongezeka kwa ufaulu wa mitihani ya Dini.
- Kuongezeka kwa idadi ya walimu wastaafu na wasiowastaafu waliotambuliwa na kujengewa uwezo
- Kuanzishwa kwa madarasa ya Dini baada ya Kipaimara kwa kila Parokia
- Kuongezeka kwa uelewa wa waamini walei juu ya imani katoliki
- Kuongezeka kwa idadi ya waamini waliopokea/ wanaopokea Sakramenti.

Mpango Mkakati wa pili

Kuimarisha utendaji wa Halmashauri ya Walei katika ngazi zote za uongozi.

Mkakati (Strategies)

Kuimarisha Utendaji wa Viongozi walei na kamati ndogo ndogo za kikatiba na zisizo za kikatiba.

Malengo Mahususi (Targets)

- Kutoa mafunzo ya uongozi kwa viongozi walei katika ngazi zote.
- Kuimarisha utendaji wa Kamati za Kikatiba na zisizo za Kikatiba katika ngazi mbalimbali
- Kutoa mafunzo ya uongozi kwa viongozi vya Vyama, Mashirika na Jumuia za Kitume

Viashiria vya Utendaji (Key Performance Indicators)

- Viongozi kuwajibika katika kutekeleza kwa wakati maagizo yanayotolewa na hierakia.
- Kuwepo na mfumo wa uandaaji na utunzaji wa Kumbukumbu mbalimbali
- Uwepo wa ratiba/kalenda za vikao na mikutano ya Halmashauri
- Kufanyika kwa Vikao kwa Mujibu wa katiba.
- Kuwepo kwa miongozo mbalimbali ya utendaji na mawasiliano bora kwa ngazi zote kwa kuzingatia muda.

Mpango Mkakati wa tatu

Kubuni mipango ya kimaendeleo na kuratibisha mambo yanayohusu mipango, uchumi na fedha.

Mkakati (Strategies)

- Kuwezesha semina za ujasiriamali kwa waamini ili wapate elimu ya kukuza uchumi wao
- Kuanzisha mradi wa ufugaji wa ng’ombe, nguruwe na kuku Kisarawe

Malengo Mahususi (Targets)

- Kutoa semina 4 za ujasiriamali kwa mwaka.
- Kutumia fursa za uwekezaji zinazijitokeza kwa kiwango cha juu
- Kutoa mafunzo juu ya mwongozo wa fedha na mali za kanisa
- Kuendeleza Ujenzi wa miundo mbinu mbalimabli katika shamba la Kisarawe kufikia mwishoni mwa Mwaka 2024.
- Ununuzi wa mifugo

Viashiria vya Utendaji (Key Performance Indicators)

- Kuongezaka kwa idadi ya waamini walei wenye uelewa wa ujasiriamali
- Kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji
- Kuhakikisha Mpango wa fedha wa Jimbo unatumika katika ngazi zote
- Kumpata Mzabuni na Mshauri kwa ajili ya Ufugaji
- Kakamilika kwa miundo mbinu ya mradi wa ufugaji.
- Mradi wa ufugaji kuanza
- Kukua kwa uchumi wa Halmashauri walei

Mpango Mkakati wa nne

Kuimarisha ufuatiliaji na tathimini ya malengo ya Mpango Mkakati

Mkakati (Strategies)

Kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango mkakati

Malengo Mahususi (Targets)

- Kufuatilia utekelezaji wa mpango mkakati mara 2 kwa Mwaka

Viashiria vya Utendaji (Key Performance Indicators)

- Kuwepo kwa madodoso ya kufanya tathimini ya utekelezaji wa Mpango Mkakati
- Kufanya ziara mbalimbali za kutathmini utendaji

Malengo ya kimkakati yatafanikiwa pale ambapo yamewekewa mikakati maalumu, shughuli husika, viashiria na Mhusika Mkuu katika kuratibisha. Kwa sababu hiyo jedwali linalofuata linatanabaisha yatakayojiri katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2023 hadi 2026. Aidha kutokana na Mpango Mkakati huu, Jimbo litaweza kuandaa mipango ya utekelezaji kwa kila mwaka

MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO MKAKATI - MALENGO MAKUU (OBJECTIVE DESCRIPTIONS) KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU (2023 HADI 2026).

Na	MIKAKATI (STRATEGIES)		MALENGO MAHUSUSI(TARGETS)	VIASHIRIA VYA UTENDAJI (KEY PERFORMANCE INDICATORS)	UTHIBITISHO /MATOKEO	MSIMAMIZI
1.	**Kuimarisha IMANI ya waamini Walei.**					
	1.1	Kuimarisha Maisha ya kitakatifu miongoni mwa walei kwa kuwahimiza kusoma neno la Mungu, Katekisimu ya Kanisa Katoliki, Mtaguso mkuu wa Vatikani na nyaraka mbalimbali za kanisa.	Uwepo wa vikundi vitatu vya kujifunza kwa undani mafundisho ya kanisa katoliki kwa kila Parokia.	Kupungua kwa idadi ya waamini walei wanaoiasi Imani Katoliki.	Idadi ya vikundi vya mafundisho ya dini vilivyoanzishwa kwa kila Parokia.	Katibu Msaidizi
				Kuongezeka kwa idadi ya waamini wakatoliki	Sensa ya waumini kila Mwaka	

				Kuimarika Zaidi kwa Imani ya waamini Walei na kuongezeka kwa miito mitakatifu	Sensa ya waamini	
				Kuongezeka kwa idadi ya washiriki kwenye Hija, Semina, warsha, mafungo na makongamano	Taarifa za mahudhurio	
				Kuongezeka kwa idadi ya waumini wanaoshiriki sakramenti mbalimbali za kanisa	Taarifa za sakramenti za kanisa	
			Idadi ya waamini wanaofuatilia Vyombo vya Habari vya kanisa kufikia kiwango cha juu.	Kuongezeka kwa idadi ya waamini wanaofuatilia vyombo vya Habari vya kanisa.	Taarifa za madodoso	

			Kuimarisha miundombinu ya maeneo ya huduma za Kiroho kama maeneo ya Hija, Makanisa na Vituo vya sala	Kuendelea kwa kituo cha Hija Pugu na kuwekeza kwa shughuli za kiibaada.	Taarifa za utekelezaji	
				Kuongezeka kwa idadi ya Makanisa.	Taarifa za Mwaka.	
	1.2	Kuongeza uelewa kwa waamini Walei kuhusiana na malezi, familia na afya kufikia kiwango cha juu.	Kuendesha semina 2 kwa mwaka zenye lengo la kuboresha uelewa kuhusiana na masuala ya malezi, familia na afya	Kuimarika kwa maadili miongoni mwa waamini walei	Taarifa za semina	Mwenyekiti
				Kuongezeka kwa idadi ya wanandoa wanaotumia mpango wa uzazi wa asili.	Taarifa za Madodoso.	

				Kupungua kwa idadi ya waamini wanaoishi Maisha ya unyuma bila sakramenti ya ndoa kwa kiwango cha juu.	Taarifa za ndoa	
			Kuhamasisha waamini kufuatilia vyombo ya Habari vya kanisa.	Kuongezeka kwa waamini wanaofuatilia Habari za kanisa kufikia kufikia kiwango cha juu	Taarifa za Madodoso.	
			Kuhamasisha waamini Walei kuwa kuwa na tiba kinga na bima za afya.	Idadi ya waamini walei wenye bima ya afya kufikia asilimia kubwa.	Taarifa za waamini walei wenye bima za afya.	
				Kupungua kwa magonjwa yasioambukizwa miongoni mwa waamini walei kwa kiasi kikubwa.	Taarfa za hali ya afya za waamini walei.	

	1.3	Kuongeza uelewa kwa waamini Walei katika masuala yanayohusu Haki, Amani, Ulinzi, Usalama na Mazingira	Kuimarisha makundi mbalimbali ya uinjilishaji kama vile vyama vya kitume, Vijana na kamati sizizo za kikatiba kwa njia ya semina 2, Hija 2 na Mafungo 2 kwa mwaka.	Kuongezeka kwa idadi ya vikundi vya uinjilishaji	Taarifa za Semina /Hija/ Mafungo zilizofanyika	Katibu
				Kuongezeka kwa uelewa wa waamini katika mambo ya Haki wajibu na sheria.	Taarifa Mbalimbali	
	1.4	Kuhimiza ufundishaji wa Elimu ya Dini Mashuleni na Vyuoni.	Utoshelevu wa mafundisho ya Dini mashuleni na vyuoni kufikia asilimia kubwa.	Mafundisho ya dini mashuleni kufanyika kwa mujibu wa ratiba	Taarifa za mafundisho ya Dini Mashuleni	Katibu Msaidizi
				Kuongezeka kwa ufaulu wa mitihani ya Dini.	Matokeo ya Mitihani ya Dini	
	1.5	Kuratibisha mafundisho ya elimu ya Dini baada ya Kipaimara	Kuwatambua walimu wakatoliki Wastaafu na wasiowastafu walio waadilifu kwa kila Parokia na kuwajengea uwezo wa kufundisha Elimu ya Dini.	Kuongezeka kwa idadi ya walimu wastaafu na wasiowastafu waliotambuliwa na kujengewa uwezo	Taarifa ya Utekelezaji	Katibu Msaidizi
			Kutoa Mafundisho endelevu ya Dini kwa watoto wote waliopata Kipaimara.	Kuanzishwa kwa madarasa ya Dini baada ya Kipaimara kwa kila Parokia	Taarifa za utekelezaji wa mafunzo	

					baada ya Kipamiara	
	1.6	Kuimarisha uinjilishaji kwa parokia zilizo pembezoni kwa lengo la kukuza Imani Katoliki	Kufanya ziara za uinjilishaji 4 kwa mwaka kwa kila Parokia za Pembezoni	Kuongezeka kwa uelewa wa waamini walei juu ya imani katoliki	Taarifa za ziara za Uinjilishaji	
				Kuongezeka kwa idadi ya waamini waliopokea/ wanaopokea Sakramenti.	Taarifa ya Sensa za waumini	

Na	MIKAKATI (STRATEGIES)		MALENGO MAHUSUSI(TARGETS)	VIASHIRIA VYA UTENDAJI (KEY PERFORMANCE INDICATORS)	UTHIBITISHO /MATOKEO	MSIMAMIZI
2	**Kuimarisha utendaji wa Halmashauri ya Walei katika ngazi zote za uongozi**					
	2.1	Kuimarisha Utendaji wa Viongozi walei na kamati ndogo ndogo za kikatiba na zisizo za kikatiba.	Kutoa mafunzo ya uongozi kwa viongozi walei katika ngazi zote.	Viongozi kuwajibika katika kutekeleza kwa wakati maagizo yanayotolewa na hierakia.	Taarifa za utekelezaji.	Katibu
				Kuwepo na mfumo wa Uandaaji na utunzaji wa Kumbukumbu mbalimbali	Kumbukumbu za mikutano.	
			Kuimarisha utendaji wa Kamati za Kikatiba na zisizo za Kikatiba katika ngazi mbalimbali	Uwepo wa ratiba/kalenda za vikao na mikutano ya Halmashauri	Kumbukumbu za Vikao na mikutano na matukio mbalimbali	
			Kutoa mafunzo ya uongozi kwa viongozi vya Vyama,	Kufanyika kwa Vikao kwa Mujibu wa katiba.	Kumbukumbu za Vikao na mikutano na	

			Mashirika na Jumuia za Kitume		matukio mbalimbali	Makamu Mwenyekiti
				Kuwepo kwa miongozo mbalimbali ya utendaji na mawasiliano bora kwa ngazi zote kwa kuzingatia muda.	Uwepo wa Katiba ya Walei na VMJ Kiwango cha utekelezaji.	

Na	MIKAKATI (STRATEGIES)		MALENGO MAHUSUSI(TARGETS)	VIASHIRIA VYA UTENDAJI (KEY PERFORMANCE INDICATORS)	UTHIBITISHO /MATOKEO	MSIMAMIZI
3	**Kubuni mipango ya kimaendeleo na kuratibisha mambo yanayohusu mipango, uchumi na fedha**					
	3.1	Kuwezesha semina za ujasiriamali kwa waamini ili wapate elimu ya kukuza uchumi wao.	Kutoa semina 4 za ujasiriamali kwa mwaka.	Kuimarika kiuchumi kwa waamini walei.	Taarifa za Semina mbalimbali	Mtunza Hazina.
				Kuongezeka kwa idadi ya waamini wanaolipa zaka na matoleo mbalimbali ya kanisa.	Taarifa za fedha	
				Kupungua kwa idadi ya waamini wanaokimbilia injili zinazohubiri utajiri wa haraka	Taarifa za sensa za waamini	
			Kutumia fursa za uwekezaji zinazijtokeza kwa kiwango cha juu.	Kuongezeka kwa miradi ya uwekezaji	Taarifa za uwekezaji	
			Kutoa mafunzo juu ya mwongozo wa fedha na mali za kanisa	Kuhakikisha Mpango wa fedha wa Jimbo unatumika katika ngazi zote	Taarifa za Utekelezaji	

	3.2	Kuanzisha mradi wa ufugaji wa ng'ombe, nguruwe na kuku Kisarawe	Ujenzi wa miundo mbinu kufanyika kwa kufikia mwishoni mwa Mwaka 2024.	Kakamilika kwa miundo mbinu ya mradi.	Taarifa ya Mradi	
			Ununuzi wa mifugo	Mradi wa ufugaji kuanza	Taarifa ya Mradi	
Na	**MKAKATI (STRATEGIES)**		**MALENGO MAHUSUSI(TARGETS)**	**VIASHIRIA VYA UTENDAJI (KEY PERFORMANCE INDICATORS)**	**UTHIBITISHO /MATOKEO**	**MSIMAMIZI**
4.	**Kuimarisha ufuatiliaji na Tathimini ya malengo ya Mpango Mkakati**					
	4.1	Kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango mkakati	Kufuatilia utekelezaji wa mpango mkakati mara 2 kwa Mwaka.	Kuwepo kwa madodoso ya kufanya tathimini ya utekelezaji wa Mpango Mkakati.	Taarifa za Utekelezaji	Kamati ya Utekelezaji
				Kufanya ziara mbalimbali za kutathmini utendaji	Taarifa za Tathimini	

SURA YA NNE

4.0 MPANGO WA FEDHA NA MAKISIO

4.1 Makisio ya mapato na matumizi

Halmashauri ya Walei Jimbo inategemea vyanzo mbalimbali vya mapato kuendesha shughuli za kuinjilisha na uendeshaji. Sehemu kubwa ya mapato yake ni kupitia sadaka za waumini kupitia Parokia za Jimbo siku ya Pentekoste.

Mapato yatakayokusanywa na Matumizi ya fedha yatategemea na mpango kazi wa mwaka utakaokuwa unaandaliwa. Gharama halisi kwa matumizi zitajionyesha kwenye mpango kazi wa mwaka.

Upo utaratibu mzuri wa kuhifadhi pesa benki kwa usalama na kisha kuzitoa kwa kutumia watia sahihi walioidhinishwa.

4.2 Ufuatiliaji na Tathimini

Mpango mkakati huu wa Halmashauri Jimbo na utekelezaji wake utaratibiwa na kufanyiwa tathimini ya utekelezaji wake. Tathimini hii itakuwa ya ndani siyo kutoka nje. Vipindi vya kufanyia tathimini itakuwa miezi sita sita, kila mwaka na mwisho wa Mpango mkakati ambao ni miaka mitatu.

Tathimini itakayo fanyika itatumia viashiria vya mawasiliano kama vilivyoainishwa kwenye jedwali la mpangokazi. Tathimini zote zitajadiliwa katika vikao mbalimbali vya kikatiba ili kuwezesha kufikia makubaliano na mapendekezo.

Baada ya mwaka kukamilika Mpango Mkakati utafanyiwa tathimini kwa kutumia viashiria na taarifa za utekelezaji zilizojadiliwa kwenye vikao husika. Kisha itaandaliwa taarifa ya mwaka na mwisho wa miaka mitatu ya utekelezaji, ikijumuisha mambo muhimu yanayosaidia, mpango utakaofuata.